**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KUTAIFA JUU YA MSWADA WA SHERIA YA KUANZISHA OFISI YA MUFTI WA MKUU ZANZIBAR NA KUWEKA USIMAMIZI BORA WA SHUGHULI ZA KIISLAM ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naanza kuwasilisha Hotuba yangu hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo kwa kutujaalia uhai na afya njema, ambayo imetuwezesha kukamilisha jukumu muhimu la Nchi yetu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu Azidi kutubariki amani na upendo, busara na hekima, pamoja na neema zake zote ambazo kwa hakika sisi ni wahitaji kutoka kwake.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia, kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati yetu katika Baraza hili tukufu kwa ajili ya kuuchangia na kuuboresha Mswada huu wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na Kuweka Usimamizi Bora wa Shughuli za Kiislam Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie hekima na busara katika kutekeleza majukumu yako ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa dhati kabisa, natoa shukurani zetu maalum kwa uongozi mzima wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mashirikiano yao makubwa

wanayoipatia Kamati na kupelekea kazi ya kuupitia na kuujadili Mswada huu kuwa nyepesi kwetu.

**Mheshimiwa Spika**, pia, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano yao makubwa waliyotoa kwangu na juhudi zao wakati wa kuujadili kwa kina Mswada huu.

Naomba sasa kwa ruhusa yako niwatambulishe Wajumbe wa Kamati hii kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Machano Othman Said | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Haji Jecha Salum | Katibu |
| 9. | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |
| 10. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo ambayo Kamati yetu imeyafanya na pia, naomba kuwaeleza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ya kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi tu na msisitizo wa baadhi ya vifungu ambavyo vimependekezwa kufanyiwa marekebisho na Kamati kutokana na ubora wa mswada wenyewe. Hivyo, maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yamo katika marekebisho ya Kamati

ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa ili kujisomea kwa ufafanuzi na ufahamu zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri katika Kifungu cha 2 cha Mswada huu kurekebishwa katika tafsiri ya neno "*Maahad*", kwa kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

*"'Maahad' maana yake ni chuo kinachotoa elimu ya Kiislam kwa mfumo rasmi kuanzia ngazi ya msingi, sekondari hadi stashahada;"*;

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati inapendekeza kifungu cha 15(3) kufutwa na kuandikwa upya ili kuweka usahihi wa mpangilio wa sentensi kama ifuatavyo:

*"(3) Katibu Mtendaji atakuwa Mwenyekiti wa Kamati".*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri marekebisho katika kifungu cha *17* kwa kwa kuongezwa maneno "*na Afisa Masuul*" katika kifungu kidogo cha *(1)* baina ya neno "*Mkuu*" na "*wa*" na kuyafuta maneno hayo katika kifungu kidogo cha *(2)* yaliopo baina ya neno "*Mtendaji*" na "*atawajibika*";

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, Kamati inashauri kufutwa kwa kifungu cha *42* kwa vile tayari jukumu lililoelezwa katika kifungu hicho la kutangaza kuandama kwa mwezi tayari limeshaelezwa katika kifungu cha *9(1)(d)* kinachohusiana na kazi za Mufti Mkuu.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu imebaini kuwa skuli mbali mbali huweka utaratibu wa kuwataka wanafunzi wake ambao ni watoto wetu kuhudhuria katika masomo ya ziada na kupelekea watoto hao kushindwa kuhudhuria katika madrasa na kuwakosesha elimu ya dini ya Kiislam, hivyo, Kamati inaishauri Ofisi ya Mufti kukaa pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kujadiliana na kuweka utaratibu mzuri utakaowawezesha watoto wetu kuhudhuria skuli na madrasa ili waweze kuwa na maadili mema na kunufaika na elimu zote mbili.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, Kamati yetu imegundua kuwa, ugawaji wa sadaka na misaada ya kheri haigaiwi kwa ulingano sawa nchini, hivyo, Kamati inaishauri Ofisi ya Mufti kuwa na utaratibu mzuri wa kugawa sadaka na misaada ya heri kwa wale wote wanaohusika kwa usawa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu, pia, imebaini kwamba, kunakosekana nidhamu katika kukosoana miongoni mwa masheikh ambapo hupelekea kuvunjiana heshima, hivyo, Kamati inaishauri Ofisi ya Mufti kuweka utaratibu mzuri utakaotumika katika kukosoana na kuweka adhabu kwa wale wote watakaokwenda kinyume na utaratibu utakaowekwa.

**Mheshimiwa Spika,** nina imani kuwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu watakubaliana na maoni yote ya yaliyotolewa na Kamati kupitia Mswada huu, kwa kubaini maeneo mbali mbali ya kuishauri Serikali kuhusu utekelezaji bora wa Sheria inayotarajiwa kutungwa amabayo itatoa fursa kwa taasisi zinazohusika na sheria hizi kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati yetu inawaomba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwamba Mswada huu uliombele yetu waujadili na kuuchangia ipasavyo na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria ambayo itaziwezesha taasisi hizi kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Ahsante,

.............................

*(Hassan Khamis Hafidh)*

**Mwenyekiti,**

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

Baraza la Wawakilishi Zanzibar